Utangulizi kwa Faragha

Washiriki wataangazia hali yao ya faragha ya kibinafsi na athari yake katika maisha yao. Washiriki watazingatia aina ya maelezo ambayo wangependa kuweka kuwa faragha na miktadha ambapo hawatashiriki maelezo maalum.

Nyenzo

Kitini cha Mchezo wa Faragha

Je, “Faragha” ina Maana Gani Kwako?

Mchezo wa Faragha

Mwingiliano wa Darasa

Sambaza Kitini cha Mchezo wa Faragha.

Ambia Wanafunzi Wako

Wewe hufanya maamuzi kuhusu faragha yako kila siku, hususan unapoenda mtandaoni na kutumia kifaa chako cha mkononi au vifaa vingine vya kidijitali. Mara nyingi, huenda huchukui muda mrefu ukifikiria kuhusu kila mojawapo ya maamuzi haya. Ila maamuzi hayo yote huwa ndio uelewa wako mahususi wa faragha.

Faragha ni uwezo wa kudhibiti mambo ambayo watu wengine wanajua kukuhusu. Unaweza kufanya hivi kwa kusema mambo fulani kukuhusu (kama kuwajulisha watu wengine anwani yako au mambo unayopenda kufanya kujiburudisha) au kufanya mambo fulani pamoja a watu wengine (kwa mfano kuenda dukani pamoja na marafiki zako na kuchagua vitu unavyohitaji zaidi). Faragha ni muhimu uwe chumbani pamoja na watu wengine au uwe unazungumza nao mtandaoni.

Faragha hutegemea maamuzi yako binafsi. Maana ya faragha kwako na familia yako huenda ikawa tofauti na ilivyo kwa watu wengine kwenye kikundi hiki na familia zao. Ikiwa tutakuwa na uelewa wa yale mambo tunayoyathamini kuwa ya faragha na jinsi tabia zetu tukiwa mtandaoni hukuza faragha yetu, tutaweza kufanya maamuzi bora zaidi kuhusu aina ya faragha tunayotaka.

Sasa tutashiriki kwenye mchezo wa haraka kuhusu faragha [tafadhali rejelea Kitini cha Mchezo wa Faragha] utakaokusaidia kuzingatia jinsi ya kufikiria na kuhisi kuhusu faragha. Kila mmoja atajaza kitini chako, utatembea nacho chumbani na utajitambulisha kwa mshiriki mwingine. Kisha wewe pamoja mshiriki huyo mwingine mtaulizana maswali kuhusu maelezo yaliyo kwenye kitini. Usionyeshe kitini chenyewe kwa washiriki wengine! Kitini chako hakitakusanywa mwishoni mwa shughuli — uko huru kuenda nacho nyumbani au kukitupa mbali iwapo utapenda.

Katika kila mazungumzo, kila mshiriki lazima ashiriki angalau majibu matatu ya maswali ambayo mshiriki mwenzake aliuliza. Washiriki wanaweza kuchagua kushiriki zaidi ya majibu matatu. Washiriki wanaweza kuchagua ni maelezo yepi matatu au zaidi wanaweza kushiriki. Je, kila mshiriki atashiriki maelezo kiasi gani? Je, kila mshiriki atashiriki maelezo yepi? Hebu tutembee na tuzungumze!

Mwingiliano wa Darasa

Wape washiriki kitini ili wajaze. Kisha uwape washiriki dakika 15 kutembea chumbani na kutagusana na wenzao. Baadaye, jiunge na kikundi kizima kwenye mjadala

ukitumia maswali yafuatayo. Hatimaye, hakikisha kwamba ama washiriki wametupa vitini vyao au wameenda navyo – wewe kama mshauri hufai kukusanya vitini hivyo.

Mjadala

Uliza Wanafunzi Wako

Je, kuna maelezo fulani ya kweli ambayo hukushiriki na mtu yeyote? Je, ni zipi? Kwa nini?

Je, ulishiriki maelezo yepi ya ukweli? Kwa nini?

Je, kila mmoja alifanya maamuzi sawa na ya wenzake kuhusu maelezo ya kushiriki? Kwa nini / kwa nini hawakufanya hivyo?

Kulingana na mtu unayeshiriki naye, je ni nini unaweza kushiriki zaidi au chache kuyahusu ya aina hii ya maelezo? Je, unaweza kushiriki kuyahusu wakati gani?

Je, kuna chochote ulichoshiriki wakati wa shughuli hii ambacho huenda usingeshiriki na watu wote unaowajua? Kwa nini usingeyashiriki?

Je, aina hii ya maelezo ni ya umma? Je, ni ya faragha? Kwa nini? Je, hali hii ni sawa kwa kila mtu?

Ambia Wanafunzi Wako

Jinsi ulivyosikia sasa hivi, watu walifanya maamuzi tofauti kuhusu maelezo ya kushiriki na yale ambayo hawashiriki. Pia, walikuwa na sababu mbalimbali za kufanya maamuzi yao.

Tulichofanya sasa ni mchezo. Lakini huwa tunafanya aina sawia na hii ya maamuzi kila siku katika uhalisia wa maisha. Huwa tunaamua ikiwa tutachapisha picha mahususi kwenye mitandao ya kijamii au la. Tunaamua ikiwa tunahitaji maelezo mahususi ya anwani au la, kama vile anwani zetu za barua pepe zinazopatikana kwenye umma katika akaunti zetu za mitandao ya kijamii. Maamuzi yetu yanaweza kuwa tofauti na yale ya rafiki yetu au hata maamuzi yetu ya mwezi uliopita. Hata ikiwa tutafanya maamuzi sawa katika hoja mbili tofauti kwa wakati mmoja, huenda sababu zetu zikawa tofauti.

Maamuzi haya na sababu hizi zinawakilisha uelewa wetu wa kibinafsi kuhusu faragha.

Kwa maelezo mepesi, faragha hurejelea jinsi tunavyochagua kushughulikia maelezo kutuhusu. Maelezo haya yanaweza kujumuisha sehemu ya utambulisho, shughuli, mapendeleo, kaida zetu na nyenzo nyingine za maisha yetu. Katika ulimwengu wa sasa wa kidijitali, kuna nafasi nyingi zaidi kuliko hapo awali za kushiriki na watu wengine maelezo kutuhusu. Kwa hivyo ni muhimu kwamba tuanze kuwa na uelewa

wetu binafsi wa faragha na kwamba tufikirie kuhusu ikiwa tunaridhika na uelewa huo au la.

Uliza Wanafunzi Wako

Kulingana na tabia yako katika mchezo kuhusu faragha, na vilevile tabia yako katika maisha ya kila siku, je unawezaje kufafanua faragha? Kwa nini?

Je, maelezo yote ya faragha huwa pia siri?

1. Sivyo haswa. Kwa mfano, tarehe ya siku yako ya kuzaliwa huenda sio siri jinsi maelezo kwenye shajara yako yalivyo. Kuna watu wengi ulimwenguni ambao wana fahamu tarehe ya siku yako ya kuzaliwa na wale wanaohitaji kuijua, kama vile wazazi wako/ watunzaji au daktari wako. Lakini kwa sababu jambo fulani si la siri, bado unaweza kulichukulia kuwa la faragha. Watu wengi wasingependa kila mtu afahamu tarehe yetu ya siku ya kuzaliwa kwa sababu tunazingatia maelezo hayo kama ambayo watu walio karibu nasi pekee au watu walio na sababu maalum ya kuyafahamu pekee ndio wanafaa kuyafahamu. Aina hizi za maamuzi kuhusu ni nani anafaa kufahamu jambo kutuhusu, lini na kwa nini ndiyo viungo muhimu vya faragha.

Uliza Wanafunzi Wako

Je, kuna mambo mengine ambayo sio siri haswa ambayo huenda bado ukataka kuweka faraghani ili yasijulikane na watu usiowafahamu vyema / watu ambao umekutana nao hivi karibuni?

1. Nambari za simu, anwani za barua pepe, picha, video n.k

Je, kuna mambo fulani huenda ungependa kuficha ili wazazi wako / watunzaji au marafiki zako wasifahamu? Je, walimu wako au washauri wako wengine?

1. Matokeo yako shuleni, akaunti yako ya Instagram na shajara yako.

Je, ulijifunza chochote kile kuhusu uelewa wako wa kibinafsi kuhusu faragha ambacho kilikushangaza?

Ambia Wanafunzi Wako

Unaweza kuchukua Mchezo wa Faragha uende nayo baada yetu kumaliza shughuli ya leo! Kwa vile sasa unafikiri zaidi kuhusu faragha, utaona nafasi nyingi zaidi za kufanya chaguzi kila siku ambapo unatekeleza uelewa wako wa kibinafsi kuhusu faragha.

Kazi

Kazi

Ambia Wanafunzi Wako

Sasa tunaenda kuangazia zaidi uelewa wako binafsi wa faragha.

1. Tafuta mifano mitatu kutoka mtandaoni ambapo mtu alishiriki au kuchapisha jambo ambalo wewe binafsi ungeweka kuwa faragha. Haya yanaweza kutoka kwa watu mashuhuri, wanasiasa au watu mashuhuri katika ulingo wa biashara, au unaweza kutafuta kupitia alama ya reli au kupitia utafutaji jumla mtandaoni ili upate mifano ya hapa na pale. Jaribu utafute rasilimali mbalimbali kuhusu mada mbalimbali (m.f picha, video, machapisho ya matini kama vile maoni ambayo mtu alitoa kwenye mtandao wa kujamii na / au jukwaa la habari).

2. Kwa mfano, andika maelezo kwenye aya moja kuhusu ni kwa nini wewe ungechagua kuweka maelezo haya kuwa ya faragha. Kwenye aya yako, tafadhali eleza ikiwa/ jinsi maoni yako ya kibinafsi kuhusu kushiriki maelezo haya hubadilika kwa kutegemea muktadha (m.f watu unaotagusana nao, idadi ya watu wanaohusika katika mtagusano huo, madhumuni na lengo, mazingira [shuleni dhidi ya nje ya shule]).

Utoaji

Wape washiriki dakika 40 kukamilisha kazi.

Rasilimali hii ya mafunzo inapatikana kwa Vijana na Vyombo vya Habari katika Kituo cha Berkman Klein kwa Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Berkman Klein chini ya leseni ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0 International, bora tu utoe sifa kwa Vijana na Vyombo vya Habari kama chanzo asili na ushiriki kazi nyingine za ziada chini ya masharti yayo hayo.Hizi pamoja na rasilimali nyingine za mafunzo pia zinapatikana mtandaoni kwenye Jukwaa la Rasilimali ya Kusoma na Kuandika Kidijitali la Berkman Klein.